# CHAMA CHA KULINDA NA KUTETEA HAKI ZA WALIMU TANZANIA "CHAKUHAWATA"

## KATIBA YA CHAMA YA MWAKA 2015

## TOLEO LA KWANZA JULY 2015

# CHAMA CHA KULINDA NA KUTETEA HAKI ZA WALIMU TANZANIA

(CHAKUHAWATA)

**Makao makuu ya chama:**

Makao makuu ya chama yapo Kigoma mjini

Mawasiliano:

Barua pepe: chakuhawata.kigoma@yahoo.com

Au chakuhawatakigoma@gmail.com

## YALIYOMO


**SEHEMU YA KWANZA**

Utangulizi

**SEHEMU YA PILI**

1. Jina la chama
2. Anuani ya chama
3. Kauli mbiu ya chama
4. Madhumuni ya chama

**SEHEMU YA TATU**

**UANACHAMA**

5. Mwanachama

**SEHEMU YA NNE**

**HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA**

6. Haki za mwanachama
7. Wajibu wa mwanachama
8. Kujiunga na chama
9. Ukomo wa Uanachama

## SEHEMU YA TANO

### VIKAO VYA CHAMA

10. Vikao vya chama.

11. Vikao vya Tawi

12. Wajibu wa vikao vya Tawi

13. Wajibu wa viongozi wa Tawi

14. Vikao vya wilaya

15. Wajibu wa vikao vya wilaya

16. Wajibu wa viongozi wa wilaya

17. Vikao vya Taifa

18. Wajibu wa vikao vya Taifa

19. Wajibu wa viongozi wa Taifa

20. Wadhamini wa chama

21. Kitengo cha walimu wanawake

22. Utaratibu wa vikao vya chama vitakavyoitishwa

23. Namna ya viongozi wa chama watakavyopatikana

SEHEMU YA SITA

24. Fedha za chama

25. Bajeti ya kila mwaka

26. Mali za chama

SEHEMU YA SABA

27. Mabadiliko ya katiba

28. Kanuni za chama

29. Kukaimu uongozi

30. Kujaza nafasi zilizo wazi katika chama

31. Kufutwa kwa chama

32. Mgomo

33. Kuungana na kuunda shirikisho

SEHEMU YA NANE

34. UFAFANUZI AU FASILI

## SEHEMU YA KWANZA.

## UTANGULIZI

Kwa kuwa sisi walimu na wanataaluma wote wa taaluma ya Ualimu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunao wajibu mkubwa wa kuelimisha jamii ya watanzania na kutayarisha viongozi na wanataaluma wazuri wa Tanzania ya leo na kesho. Kwa kuwa kazi ya Ualimu inahitaji elimu, ujuzi na uzalendo kwa ujumla.

Aidha chama hiki si chama cha kujitafutia kipato kwa maslahi ya mtu binafsi kwa kuwa chama hiki hakiwezi kushughulikia utetezi wa wafanyakazi na kuendesha biashara.

Kwa kuwa mwalimu ni mfanyakazi kama walivyo wafanyakazi wa kada nyingine nchini, anahitaji kupata haki zote zinazomstahili kama zilivyoelezwa katika Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hivyo basi, walimu tumeamua kuungana na kuanzisha chama cha wafanyakazi kitakachosimamia haki na wajibu wa mwalimu bila ubaguzi wa rangi, kabila, dini, ujimbo wala jinsia na kuhakikisha kuwa waajiri nao wanatimiza wajibu wao kwa waajiriwa.

## SEHEMU YA PILI

### 1. JINA LA CHAMA

JINA LA CHAMA NI: CHAMA CHA KULINDA NA KUTETEA HAKI ZA WALIMU TANZANIA (CHAKUHAWATA)

### 2. ANUANI:

KATIBU MKUU,

CHAMA CHA KULINDA NA KUTETEA HAKI ZA WALIMU TANZANIA

[CHAKUHAWATA]

SLP 497,

KIGOMA - TANZANIA

### 3. KAULI MBIU YA CHAMA

**"Hakuna haki bila wajibu" Na "Hakuna wajibu bila haki"**

### 4. MADHUMUNI YA CHAMA

a. Kukuza haiba ya kazi ya ualimu, mazingira bora ya kazi, vivutio na malipo halali kwa kazi yake na kazi za ziada kwa mujibu wa sheria na kuhakikisha kwamba mwalimu ana fursa ya kujiendeleza kwa kadri ya uwezo wake katika fani mbalimbali.

b. Kumuandaa kiuzalendo mtoto na kijana wa Tanzania kwa kumlea katika maadili mema na kujihusisha kikamilifu katika ustawi na maendeleo ya jamii.

c. Kusimamia na kutetea sera husika kuhusu walimu wanawake, makundi maalumu katika afya,maumbile na vikwazo mbalimbali katika maisha na utendaji wao kwa kuzingatia haki na sheria.

d. Kuhimiza weledi kwa watendaji katika Taasisi mbalimbali za elimu-zinazojihusisha na ufundishaji na ujifunzaji.

e. Kuwa na vikao vya mara kwa mara kwa mujibu wa katiba na wakati wowote

inapobidi kwa ajili ya kufanya tathmini za kitaaluma na kujenga mahusiano mema.

f. Kwa kuwa chimbuko la taaluma zote ni ualimu, chama kitahakikisha kuwa Ualimu ni miongoni mwa

taaluma muhimu katika jamii na si kutumia neno "Ualimu ni Wito" kumkandamiza mwalimu.

g. Kuhakikisha kuwa wote wanaohusiana na ajira ya Ualimu wanazingatia sheria za kazi, na kutotumia nyaraka au mikataba kandamizi katika kumhudumia

mwalimu ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima kati ya waajiri na waajiriwa.

h. Kuhakikisha kwamba wanachama ni majemedari wa kupambana na rushwa na aina zote za uonevu kwa vitendo na hawajihusishi na mambo hayo katika shughuli zao za kila siku.

i. Kuhakikisha kuwa serikali inawahusisha kikamilifu wadau wote wa elimu kabla ya kufanya mabadiliko yoyote ya kisera katika

elimu kwa ngazi zote na serikali kujihusisha moja kwa moja katika kuandaa vitendea kazi vya elimu ili kuinua ubora wa elimu nchini.

j. Kuhimiza waajiri kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria ya nchi na kutambua njia zote halali za kudai haki zinazowahusu waalimu katika utekelezaji wa majukumu yao.

k. Kuhakikisha uwepo wa mahusiano mazuri kati ya mwalimu na mwalimu, mwalimu na mwajiri kwa kujihusisha katika kusuruhisha migogoro mahali pa kazi.

l. Kuwaelimisha walimu wanachama kuhusu haki na wajibu wao wa msingi, kanuni na taratibu za kazi na njia halali za kuzidai inapobidi bila kuvunja sheria za nchi.

m. Kuhakikisha kuwa wanachama wanaepuka ubaguzi wa aina yoyote ikiwa ni pamoja na ubaguzi wa rangi, kabila, udini, jinsia, ujimbo au utaifa wa mtu.

n. Kuwa na ushirikiano na vyama vingine vya wafanyakazi ndani na nje ya nchi kwa manufaa ya wanachama na Taifa kwa ujumla.

o. Kuhimiza wanachama kujikomboa kiuchumi kwa kuanzisha vyama vya ushirika (SACCOS) na kuhakikisha kuwa mapato yanayopatikana yanawanufaisha wanachama wenyewe ikiwemo michango na misaada mbalimbali kutoka kwa wahisani wa ndani na nje ya nchi.

p. Kuwatambua walimu wastaafu kama wanachama na hazina muhimu kwa chama na taifa na kuhakikisha kuwa wanashirikishwa katika shughuli zote za chama.

q. Kwakuwa chama kinahimiza uzalendo, Kiswahili kama sehemu ya utamaduni wa mtanzania, kitakuwa ndio lugha muhimu itakayotumika katika vikao na mikutano ya ndani na nje ya nchi, bila kudharau lugha nyingine za kimataifa.

r. Pamoja na yote hayo yaliyotajwa hapo juu A-Q, chama hiki hakikuanzishwa kwa ajili ya maslahi binafsi, hivyo hakita jishughulisha na shughuli zozote za kibiashara.

## <u>SEHEMU YA TATU.</u>

## UANACHAMA.

### 5. MWANACHAMA

**Sifa za mwanachama;**

i) Ni mwalimu yeyote mwenye cheti halali cha ualimu au leseni ya kufundishia.

ii) Awe mwadilifu na mwenye haiba ya ualimu.

iii) Awe raia wa Tanzania na kama si raia wa Tanzania awe anafanya kazi kwa mujibu wa sheria za nchi.

iv) Awe ni mwenye kulipa ada ya chama kila mwezi

## SEHEMU YA NNE.

### HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA

### 6. HAKI ZA MWANACHAMA

i) Kila mwanachama anayo haki ya kuchagua na kuchaguliwa katika ngazi moja ya Uoñgozi.

ii) Kujitetea au kutoa maelezo katika sehemu au chombo husika dhidi ya tuhuma inayomkabili.

iii) Ana haki ya kukata rufaa katika ngazi ya juu endapo hatakuwa ameridhika na maamuzi yaliyotolewa dhidi yake, endapo tatizo litakuwa ni la viongozi wakuu wa Kitaifa, kamati tendaji ya Taifa itakuwa na uwezo wa kuonya, kusimamisha na kutoa mapendekezo kwa mkutano mkuu wa Taifa kwa maamuzi zaidi.

iv) Kutetewa na chama kuhusu maslahi yake chini ya kauli mbiu "hakuna haki bila wajibu na hakuna wajibu bila haki"

v) Kwa kuwa chama kitamiliki mali zisizoondosheka na zinazoondosheka, mwanachama atahusika moja kwa moja na umiliki wa mali hizo na kufaidi matunda yote yatokanayo na mali hizo.

vi) Kutoa maoni au mapendekezo juu ya mabadiliko yoyote ya katiba ya chama ikibidi hata kwa kura za maoni.

vii) Kuelimishwa na kuelimisha kuhusu haki za mwanachama.

viii) Haki zingine za mwanachama zitatolewa kama inavyoelekezwa katika kanuni upande wa huduma za kijamii.

## 7. WAJIBU WA MWANACHAMA

i) Kulipa ada ya Uanachama kwa kila mwezi kupitia mshahara wake kiasi cha shilingi **ELFU TANO TU** (5000/=). Na kwa wale ambao si wafanyakazi wa serikali wakiwemo walimu wastaafu watalipa ada kwa kupeleka wao wenyewe kwa katibu wa tawi husika au kuingiza moja kwa moja kwenye akaunti ya

chama na kupeleka stakabadhi ya malipo kwa katibu wa tawi husika.

ii) Kushiriki vikao vya chama vinavyomhusu.

iii) Kutekeleza maamuzi halali ya chama.

iv) Kuwajibika kwa mwajiri kwa mujibu wa sheria za kazi ili kuongeza tija na ufanisi mahali pa kazi.

v) Kutambua haki zake ndani ya chama na ndani ya ajira yake kwa mujibu wa sheria za kazi.

vi) Kuhakikisha uhai wa chama kwa kukilinda katika misingi ya kidemokrasia.

vii) Kutunza siri na mali za chama wakati wote.

## 8. KUJIUNGA NA CHAMA.

i) Mwanachama atapatikana kwa njia ya kuandika barua ya kuomba uanachama na ;

ii) atajaza fomu maalum TUF6 (yaani Trade Union Form no. 6)

## 9. UKOMO WA UANACHAMA

i) Kujiuzulu

ii) Kutoa siri za chama au kuhujumu mali za chama

iii) Akiacha au kufukuzwa uanachama, au kuachishwa kazi kwa vitendo ambavyo vinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Isipokuwa walimu wastaafu ambao ni wanachama wa chama hiki (CHAKUHAWATA)

iv) Akifariki dunia

v) Asipolipa ada kwa muda wa miezi sita (6) mfululizo tangu alipopewa taarifa juu ya kutolipa kwake ada ya uanachama.

vi) Makato halali ya ada ya uanachama hayatarejeshwa iwapo uanachama wake utakuwa umekoma kwa mujibu wa katiba hii.

## SEHEMU YA TANO

### 10. VIKAO VYA CHAMA.

i) Kwa vikao vyote vya chama vitahesabika kuwa ni halali kufanyika endapo wajumbe husika wakikao watafikia theluthi mbili (2/3) ya idadi ya wajumbe wote wa kikao katika ngazi husika.

ii) Mkutano mkuu wa chaama katika ngazi husika utaitishwa kwa kutoa taarifa ya kikao ya siku ishirini na nane (28) kabla ya siku ya kikao husika isipokuwa vikao vyote vya dharula.

### 11. VIKAO VYA TAWI

**i) Muundo wa tawi:**

Tawi litaundwa na wanachama wasiopungua kumi (10) walio katika kata za utawala wa kiserikali. Hivyo tawi litaundwa na jumla ya wanachama wote walio katika kata.

**ii) Mkutano mkuu wa tawi**

Mkutano mkuu wa tawi utafanyika mara moja kwa mwaka kwa kuwakutanisha wanachama wote walio katika tawi. Mkutano mkuu wa tawi utakuwa na wajumbe wafuatao:

a) Mwenyekiti w a tawi

b) Katibu wa tawi

c) Mweka hazina wa tawi

d) Mwakilishi mwanamke wa tawi

e) Mwakilishi wa walimu walemavu katika tawi

f) Wajumbe wengine wa kikao cha juu walio katika tawi

g) Wanachama wote walio katika tawi

**iii) Tarehe ya mkutano mkuu wa tawi**

Tarehe ya mkutano mkuu wa tawi itapangwa na kamati ya utendaji ya tawi.

**iv) Vikao vya dharura vya tawi:**

Vikao vyote vya dharura vitaitishwa wakati wowote kwa utaratibu ufuatao:

a) Kulingana na dharura yenyewe itakayokihusu chama

b) Kwa kuombwa na wanachama

wasiopungua theluthi mbili (2/3) ya wanachama wote baada ya kujiorodhesha majina yao na sahihi zao.

c) Vikao vyote vya dharura na visivyo vya dharura vitaitishwa kwa kuzingatia akidi ya theluthi mbili (2/3) ya wanachama wote katika ngazi husika.

## 12. WAJIBU WA VIKAO VYA TAWI

**(i)** Mkutano mkuu wa Tawi utakuwa na wajibu ufuatao;

a) Kupokea na kujadili kazi za chama kwa kipindi cha mwaka mmoja

b) Kufanya tathmini ya shughuli zote zilizofanywa na chama kwa kipindi cha mwaka mmoja.

c) Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya chama kwa kipindi cha mwaka mmoja.

d) Kuandaa mpango kazi wa chama kwa mwaka mzima.

e) Kufanya uchaguzi wa wajumbe watatu kwenda katika mkutano mkuu wa wilaya.

f) Kufanya uchaguzi wa viongozi wa ngazi ya tawi na wawakilishi wa kamati mbalimbali katika tawi.

**(ii) Kamati ya Utendaji ya Tawi**

(a) Kamati ya utendaji ya tawi itakutana mara nne (4) kila mwaka (yaani kila robo mwaka mara moja).

(b) Tarehe ya mkutano wa kamati ya utendaji ya tawi itapangwa na katibu wa tawi kwa kushirikiana na mwenyekiti wa tawi.

**(iii) Wajumbe wa kamati ya Utendaji ya tawi**

Kamati ya utendaji ya tawi itakuwa na wajumbe wafuatao;

(a) Mwenyekiti wa tawi

(b) Katibu wa tawi

(c) Mweka hazina wa tawi

(d) Mwakilishi mmoja kutoka kila shule au taasisi iliyo katika tawi.

(e) Wajumbe wengine wa vikao vya juu vya chama walio katika tawi

(f) Mwakilishi mmoja wa walimu wanawake katika tawi.

(g) Mwakilishi mmoja wa walimu walemavu katika tawi

**(iv) Wajibu wa Kamati ya utendaji ya tawi:**

Kamati ya utendaji ya tawi itakuwa na wajibu ufuatao;

a) Kupokea na kujadili taarifa za kazi za chama kwa kila miezi mitatu(3) au (1/4 mwaka)

b) Kufanya tathmini ya shughuli za chama zilizofanywa kwa kipindi cha miezi (3) au robo mwaka

c) Kupokea taarifa ya mapato na matumizi na kuijadili kwa kipindi cha miezi mitatu (3) (kila baada ya miezi mitatu)

d) Kuandaa mpango kazi wa chama kila baada ya miezi mitatu (3)

e) Kujaza nafasi zilizo wazi za viongozi katika tawi

f) Kuandaa ajenda za mkutano mkuu wa tawi.

## 13. WAJIBU WA VIONGOZI WA TAWI

### (i) Mwenyekiti wa Tawi

(a) Ndiye kiongozi mkuu wa chama katika tawi husika na msemaji mkuu katika tawi

(b) Kuongoza vikao vya chama katika tawi na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya tawi.

### (ii) Katibu wa Tawi.

a) Mtendaji mkuu wa shughuli za chama katika tawi husika.

b) Kuitisha vikao vya chama kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa tawi.

c) Kuandaa na kutoa taarifa za shughuli za chama kwa kipindi husika.

d) Kuwa katibu wa vikao vyote vitakavyofanyika katika tawi husika, pia kusimamia shughuli zote za uendeshaji na kufuatilia mapato na matumizi ya chama.

e) Kutunza kumbukumbu za vikao vya chama katika tawi na kumbukumbu zingine muhimu za chama.

### (iii) Mweka hazina wa Tawi

a) Kutoa taarifa za fedha za chama katika vikao vya tawi

b) Kufuatilia na kuweka kumbukumbu za mapato na matumizi ya fedha za chama katika tawi.

c) Atawajibika kutoa taarifa za fedha kwa uongozi wa wilaya

## 14. VIKAO VYA WILAYA

### (i) Mkutano mkuu wa wilaya

Mkutano mkuu wa wilaya utafanyika kila baaada ya mwaka mmoja, pia mkutano mkuu wa wilaya utakuwa na wajumbe wafuatao:

a) Mwenyekiti wa Wilaya

b) Katibu wa Wilaya

c) Mweka hazina wa Wilaya

d) Wenyeviti wote wa matawi

e) Makatibu wote wa matawi

f) Waweka hazina wote wa matawi

g) Mjumbe mmoja kutoka kila tawi

h) Mwakilishi wa kitengo cha walimu wanawake na mwakilishi wa kitengo cha walimu walemavu

i) Wawakilishi wawili wa walimu wanachama wastaafu, mmoja awe mwanamke.

### (ii) Kamati ya Utendaji ya Wilaya

Kamati ya utendaji ya wilaya itakutana mara mbili kwa mwaka. Pia kamati ya utendaji ya wilaya itakuwa na wajumbe wafuatao;

a) Mwenyekiti wa wilaya

b) Katibu wa wilaya

c) Mweka hazina wa wilaya

d) Mwakilishi wa walimu wanawake.

e) Mwakilishi wa walimu walemavu

f) Mjumbe mmoja kutoka kila tawi

**(iii) Vikao vya dharura.**

Vikao vyote vya dharura vitaitishwa wakati wowote.

a) Kulingana na dharura yenyewe itakayo kihusu chama

b) Kwa kuombwa na wanachama wasio pungua theluthi mbili (2/3) ya wanachama wote baada ya kujiorodhesha majina yao na sahihi zao.

c) Vikao vyote vya dharura na visivyo vya dharura vitaitishwa kwa kuzingatia akidi ya theluthi mbili (2/3) ya wanachama wote katika ngazi husika.

## 15. WAJIBU WA VIKAO VYA WILAYA

### (i) Mkutano mkuu wa wilaya;

Mkutano mkuu wa wilaya utakuwa na wajibu ufuatao:-

a) Kupokea na kujadili taarifa za wilaya kwa kipindi cha mwaka mmoja.

b) Kupokea taarifa ya mapato na matumizi ya fedha ya chama kwa kipindi cha mwaka mmoja (1) kama itakavyowasilishwa na kamati ya utendaji ya wilaya.

c) Kuchagua viongozi na wawakilishi wa ngazi ya Wilaya na wawakilishi wa mkutano mkuu wa Taifa itakapofika wakati wa uchaguzi kama ifuatavyo;-

i) Mwenyekiti wa Wilaya

ii) Katibu wa Wilaya

iii) Mweka hazina wa Wilaya

iv) Mwakilishi wa walimu wanawake mmoja (1)kwenda mkutano mkuu wa taifa

v) Mwakilishi wa walimu walemavu mmoja (1) kwenda mkutano mkuu wa taifa.

vi) Mwakilishi wa walimu wanachama wastaafu mmoja (1) kwenda mkutano mkuu wa taifa

vii) Mwakilishi mmoja kutoka taasisi ya elimu iliyo katika kila wilaya kwenda mkutano mkuu wa taifa.

viii) Mwakilishi mmoja kwenda mkutano mkuu wa taifa

ix) Wawakilishi wawili wa walimu wastaafu mmoja awe na mwanamke katika ngazi ya Wilaya.

**(ii) Kamati ya Utendaji ya Wilaya**

Kamati ya utendaji ya wilaya itakuwa na wajibu ufuatao:-

a) Kuelekeza na kusimamia shughuli za chama ikiwa ni pamoja na mapato na matumizi ya chama katika wilaya.

b) Kusimamia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya chama

c) Kudhibiti mapato na matumizi ya fedha za chama

d) Kuandaa vikao vya mkutano mkuu wa wilaya

e) Kuandaa mikakati ya utekelezaji wa mipango ya chama kila baada ya mwaka mmoja (1)

## 16. WAJIBU WA VIONGOZI WA WILAYA

**(i) Mwenyekiti wa wilaya**

a) Ndiye kiongozi mkuu wa chama katika wilaya na msemaji mkuu wa chama katika wilaya.

b) Kuongoza vikao vya chama katika wilaya na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya wilaya

**(ii) Katibu wa wilaya**

a) Kuitisha vikao vya chama katika wilaya kwa kushirikiana na mwenyekiti wa wilaya husika

b) Kuandaa na kutoa taarifa za shughuli za chama kwa kipindi husika

c) Kuwa Katibu wa vikao vya chama vitakavyofanyika katika wilaya husika na pia kusimamia shughuli zote za uendeshaji na kufuatilia mapato na matumizi ya fedha za chama.

d) Kutunza kumbukumbu za vikao vya chama katika wilaya husika na kumbukumbu zingine muhimu za chama

**(iii) Mweka hazina wa Wilaya**

a) Kutoa taarifa ya fedha za chama katika vikao vya wilaya.

b) Kufuatilia na kuweka kumbukumbu za mapato na matumizi ya fedha za chama katika wilaya husika.

## 17. VIKAO VYA TAIFA

**(i) Mkutano mkuu wa taifa**

Mkutano mkuu wa taifa utakutana mara moja kila

baada ya miaka mitano.

Mkutano mkuu wa taifa utakuwa na wajumbe wafuatao;

a) Mwenyekiti wa taifa

b) Makamu wa mwenyekiti taifa.

c) Katibu mkuu

d) Naibu katibu mkuu taifa

e) Mweka hazina

f) Wenyeviti wote wa wilaya

g) Makatibu wote wa wilaya

h) Waweka hazina wote wa wilaya

i) Mwakilishi mmoja wa walimu wanawake kutoka kila wilaya

j) Mwakilishi mmoja katika mkutano mkuu wa taifa

k) Mwakilishi wa walimu walemavu mmoja kutoka kila wilaya.

l) Mwakilishi wa walimu wanachama wastaafu mmoja kutoka kila wilaya.

**(ii) Kamati ya Utendaji ya Taifa**

Kamati ya utendaji ya Taifa itakutana mara moja kwa mwaka. Tarehe ya kikao

itapangwa na katibu mkuu kwa kushirikiana na Mwenyekiti.

Kamati ya utendaji ya taifa itakuwa na wajumbe wafuatao;

**(a)** Mwenyekiti wa taifa

**(b)** Makamu mwenyekiti wa taifa

**(c)** Katibu mkuu

**(d)** Naibu katibu mkuu

**(e)** Mweka-hazina

**(f)** Mwakilishi mmoja kutoka kila wilaya

**(g)** Mwakilishi wa walimu wanawake mmoja kutoka kila wilaya

**(h)** Mwakilishi wa walimu walemavu mmoja kutoka kila wilaya.

(i) Mwakilishi wa walimu wanachama wastaafu mmoja kutoka kila wilaya-

**(iii) Vikao vya dharura**

Vikao vyote vya dharura vitaitishwa wakati wowote .

(a)Kulingana na dhalura yenyewe itakayo kihusu chama

(b) Kwa kuombwa na wanachama wasio pungua theluthi mbili (2/3) ya wanachama wote baada ya kujiorodhesha majina yao na sahihi zao.

(c)Vikao vyote vya dharura na visivyo vya dharura vitaitishwa kwa kuzingatia akidi ya theluthi mbili (2/3) ya wanachama wote.

## 18. WAJIBU WA VIKAO VYA TAIFA

Mkutano mkuu wa taifa utakuwa na wajibu ufuatao:-

a) Kupokea na kujadili taarifa za chama kwa kipindi cha miaka mitano (5)

b) Kupokea taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za chama kwa kipindi cha miaka mitano (5) kama itakavyo wasilishwa na kamati ya utendaji wa taifa.

c) Kuchagua viongozi na wawakilishi wa ngazi ya taifa itakapofika wakati wa uchaguzi.

d) Kufanya mabadiliko ya katiba ya chama ikiwa itaridhiwa na theluthi mbili (2/3) ya wanachama wote wanaoudhuria mkutano mkuu wa taifa.

e) Kupokea taarifa ya mipango mbalimbali ya chama na kuipitisha.

f) Kuwachagua wawakilishi wa chama katika vikao vya muungano wa vyama vya wafanyakazi ndani na nje ya nchi.

**(ii) Kamati ya Utendaji ya taifa**

Kamati ya utendaji ya taifa itakuwa na wajibu ufuatao:

a) Kuendesha na kusimamia shughuli za chama

b) Kusimamia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya chama

c) Kudhibiti mapato na matumizi ya fedha za chama

d) Kuandaa vikao vya mkutano mkuu wa chama taifa.

e) Kuchagua majina ya wajumbe watakaoweka saini katika hundi za chama taifa.

f) Kuthibitisha jina la mkaguzi wa mahesabu ya chama na watumishi wengine wa chama.

g) Kupendekeza majina ya wadhamini wa chama

h) Kuandaa mpango wa utekelezaji wa shughuli za chama kwa muda wa miaka mitano (5) kwa kila mwaka.

## 19. WAJIBU WA VIONGOZI WA TAIFA

### (i) Mwenyekiti taifa au makamu wenyekiti taifa

a) Kuongoza vikao vyote vya chama ngazi ya taifa

b) Ndiye kiongozi mkuu wa chama na msemaji wa chama

c) Makamu Mwenyekiti atafanya shughuli zote za chama wakati Mwenyekiti hayupo au hana

uwezo kiutendaji kwa mujibu wa sheria au kwa maelekezo ya mwenyekiti.

### (ii) Katibu mkuu/naibu katibu mkuu

a) Kuandaa na kuitisha vikao vyote vya chama ngazi ya taifa kwa kushirikiana na Mwenyekiti au makamu mwenyekiti.

b) Kusimamia shughuli zote za chama za kila siku

c) Ndiye Katibu wa vikao vyote vya ngazi ya Taifa

d) Atatunza kumbukumbu zote za vikao na kumbukumbu nyingine muhimu za chama.

e) Ni mkuuu wa watendaji wote wa chama.

f) Ndiye mdhibiti mkuu wa shughuli za chama/fedha na mali zote za chama kwa ngazi zote.

g) Naibu Katibu mkuu atafanya shughuli zote za katibu mkuu wakati hayupo au hana uwezo kiutendaji kwa mujibu wa sheria au kwa maelekezo ya katibu mkuu.

**(iii) Mweka hazina**

(a) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za chama na kutunza kumbukumbu za fedha akishirikiana na Katibu mkuu.

(b) Kutoa taarifa za mapato na matumizi ya chama katika vikao vya mkutano mkuu na kamati ya utendaji ya taifa.

(c) Kuweka sahihi katika hundi.

## 20. WADHAMINI WA CHAMA

(i) Wadhamini wa chama watapatikana kama ifuatavyo:-

(a) Wadhamini wa chama watakuwa ni walimu wenye taaluma ya ualimu, wenye hekima na busara na wenye maadili ya ualimu kwa ujumla.

(b) Mkutano mkuu wa taifa utawachagua wadhamini watatu kwa kuwapigia kura

(c) Wadhamini waliochaguliwa watamchagua mwenyekiti na katibu wao kutoka miongoni mwao.

(d) Wadhamini wa chama watahudhuria mkutano mkuu kama wadau wa muhimu katika chama.

(e) Taarifa za mali na fedha za chama zilizokaguliwa na wakaguzi wa ndani na nje ya chama, nakala ya taarifa hiyo itakabidhiwa kwa wadhamini wa chama. Pale ambapo

imebainika kuwa kuna ubadhilifu wa mali na fedha za chama wadhamini watachukua hatua zinazostahili.

(f) Mali na fedha za chama zitamilikiwa kwa jina la wadhamini na kuhifadhiwa na katibu mkuu. Hii ni pamoja na mikataba yote, hati na dhamana za fedha za chama.

(ii) Mdhamini atapoteza sifa za kuwa mdhamini kama ifuatavyo:-

a) Ikiwa atajiuzulu

b) Ikiwa atafukuzwa uanachama

c) Ikiwa atakosa akili timamu

d) Ikiwa atasaliti chama na kuvunja maadili ya ualimu.

e) Ikiwa atapatikana na kosa la jinai

f) Ikiwa atafariki dunia

## 21. KITENGO CHA WALIMU WANAWAKE

(i) Kutokana na umuhimu wa kipekee wa walimu wanawake katika chama kutakuwa na kitengo cha walimu wanawake. Kitengo hiki kitaundwa na walimu wanawake ambao ni wanachama katika kila ngazi kwa kuanzia tawi hadi taifa.

Kuhusu kamati zao watachaguana katika vikao vyao kila ngazi husika wakiongozwa na katibu wa ngazi husika.

(ii) Uwakilishi wa wanawake katika shughuli za chama:- Pamoja na kuwepo kwa kitengo cha wanawake, uwakilishi wa wanawake katika shughuli za chama utakuwa wa asilimia ishirini (20%) ya wanachama wote waliopo katika ngazi zote katika ngazi za uongozi.

## 22. UTARATIBU WA VIKAO VYA CHAMA VITAKAVYOITISHWA

Vikao vyote vya chama kuanzia Tawi hadi Taifa vitaitishwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

i) Kwa kutoa taarifa ya maandishi ya siku ishirini na nane (28) kabla ya tarehe ya kikao.

ii) Agenda za mkutano ziambatane na taarifa ya kikao husika.

iii) Kwa kutaja mahali mkutano utakapofanyika, muda wa kuanza, siku na tarehe ya kikao.

## 23. NAMNA YA VIONGOZI WA CHAMA WATAKAVYOPATIKANA

### (i) UCHAGUZI WA VIONGOZI

Viongozi wote katika ngazi zote za chama watachaguliwa kwa kupigiwa kura ya siri utakapofika wakati wa uchaguzi.

### (ii) MUDA WA UONGOZI

Kiongozi yeyote atakayechaguliwa katika ngazi yoyote ya uongozi atadumu katika nafasi yake kwa muda wa miaka mitano (5), isipokuwa anaweza kupigiwa kura ya kutokuwa na imani naye ikibainika kuwa amekwenda kinyume na katiba ya chama na anaweza kuchaguliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitano na baada ya mihula hiyo anaweza kuchaguliwa katika ngazi nyingine ya uongozi.

### (iii) WATENDAJI WA CHAMA.

Watendaji wakuu wa chama watakuwa makatibu wote katika ngazi husika na maafisa wengine watakaoajiriwa.

**Nyongeza,** Makatibu katika ngazi zote watachaguliwa kwanza katika mkutano mkuu wa uchaguzi katika ngazi husika na kisha ajira ya mkataba wa miaka mitano (5) kufuata katika ngazi ya wilaya au taifa.

### (iv) NAMNA YA KUWAPATA MAAFISA WA CHAMA NA KUWAONDOA KATIKA NAFASI ZAO.

Kutakuwa na maafisa wa aina mbili, wakuchaguliwa na kuteuliwa kwa mujibu wa taaluma zao na mahitaji ya ofisi.

a) Maafisa watakaochaguliwa ni kama ilivyotajwa katika ibara ya 23(ii) ya katiba hii.

b) Maofisa wa kuteuliwa kwa mujibu wa taaluma zao, watapatikana kwa kufuata utaratibu ufuatao:

i) Kutangaza nafasi za kazi kwa kubandika matangazo kwenye mbao za matangazo kwa muda wa siku thelathini (30).

ii) Waombaji wa kazi wataandika barua za maombi na kuziwasilisha kwa katibu wa chama wa ngazi husika kabla ya muda ulio tolewa kumalizika

iii) Waombaji wa kazi watafanyiwa usaili na kamati tendaji ya ngazi husika na wale wote watakaokuwa wamekidhi vigezo watajaza mikataba ya kisheria inayohusu ajira ya kazi husika.

**v) Namna watakavyo ondolewa maafisa katika nafasi zao itakuwa kama ifuatavyo:**

(a) Maofisa wa kuchaguliwa muda wao wa ajira utakoma `baada ya kipindi cha kuwa katika nafasi zao kama kilivyotajwa katika katiba hii ibara ya 23(ii)

(b) Ikiwa atathibitika kwamba amehujumu mali za chama.

(c) Kama ataonekana kuwa anamwenendo mbaya katika utendaji wake wa kila siku kiasi cha kuathiri chama.

(d) Kwa kwenda kinyume na mkataba wa ajira yake.

(e) Kama atapatikana na makosa ya jinai.

## SEHEMU YA SITA

## 24. FEDHA ZA CHAMA.

**(i) Mapato ya chama yatapatikana kwa njia zifuatazo:**

a) Ada za uanachama.

b) Misaada na ufadhili kutoka kwa wahisani mbalimbali ndani na nje ya nchi.

c) Ada ya huduma ambayo itatokana na makubaliano ya pande zote husika na kusainiwa kwake.

**(ii) Matumizi ya fedha za chama:**

Fedha za chama zitatumika kwa mambo yafuatayo:-

a) Mishahara na gharama zinginezo zinazohusu chama kwa wakati husika, ikiwa ni pamoja na posho za vikao mbalimbali.

b) Kugharamia kesi na migogoro inayohusu chama na wanachama kwa ujumla

c) Kulipa gharama na michango mbalimbali inayohusu chama ikiwa ni pamoja na kodi ya mapato

d) Kumhudumia mwanachama katika mambo ya kijamii isipokuwa yanayohusiana na starehe kwa kutegemeana na uwezo wa chama wakati huo.

e) Kuwatuza wastaafu kama itakavyoamuliwa na kikao cha kamati tendaji ya ngazi husika.

f) Yote haya yaliyotajwa katika kifungu cha (d) na (e) yatafafanuliwa katika kanuni ya chama kipengele kinachohusu huduma za kijamii.

**(iii) Utunzaji wa fedha za chama.**

a) Fedha zote za chama zitaingizwa na kutunzwa katika akaunti ya chama.

b) Wafuatao watahusika na utunzaji wa fedha za chama katika ngazi mbalimbali.

(i) Makatibu wote katika ngazi husika

(ii) Waweka hazina wote katika ngazi husika.

(iii) Wajumbe wawili na ambao sio viongozi katika ngazi husika na ambao watachaguliwa na mkutano mkuu wa ngazi husika.

c) Kamati ya utendaji katika ngazi husika itahusika na upokeaji, utunzaji na ugawaji wa fedha katika ngazi zingine.

d) Kamati ya utendaji ya ngazi husika itawasilisha hesabu zilizokaguliwa kwenye mkutano mkuu wa ngazi husika.

## 25. BAJETI YA KILA MWAKA.

Bajeti ya kila mwaka ndiyo dira ya mapato na matumizi ya chama kila ngazi.

i) Kamati tendaji ya ngazi husika itapitisha bajeti ya kila mwaka katika ngazi husika.

ii) Mapato yote ya chama yatagawanywa na kamati ya utendaji ya chama katika ngazi husika kama kanuni zitakavyoelekeza.

## 26. MALI ZA CHAMA

i) Kamati ya Utendaji itakuwa na mamlaka ya ununuzi,ugawaji na uthibiti wa mali za chama katika kila ngazi husika.

ii) Mali zote za chama zinazohamishika na zisizohamishika zitakuwa chini ya usimamizi na udhibiti wa Kamati ya utendaji ngazi husika.

iii) Endapo kamati ya utendaji itapoteza haki au kukosa sifa ya usimamizi na udhibiti wa mali za chama, mali hizo

zitabaki chini ya uangalizi na udhibiti wa wadhamini wa chama.

iv) Pamoja na hayo yaliyotajwa katika ibara ndogo (i), (ii) na (iii) hapo juu, taarifa za mapato na matumizi ya chama na taarifa nyingine zinazohusu chama zitapatikana katika tovuti ya chama ili kila mwanachama apate taarifa za chama kwa wakati na mahali popote alipo ndani na nje ya nchi.

## SEHEMU YA SABA.

### 27. MABADILIKO YA KATIBA.

i) Mabadiliko ya katiba hii yanaweza kufanywa na mkutano mkuu iwapo theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wote wa mkutano mkuu watakubali mabadiliko hayo.

ii) Mabadiliko yoyote ya Katiba lazima yatolewe taarifa kwa katibu mkuu siku tisini (90) kabla ya kufunguliwa kwa mkutano mkuu ambao utajadili mapendekezo hayo.

### 28. KANUNI ZA CHAMA

i) Chama kitakuwa na kanuni za msingi ambazo zitaendana na katiba ya chama, pale ambapo patakuwa na utata katiba itazingatiwa zaidi.

ii) Kanuni za chama zitatungwa na kamati ya utendaji ya taifa na kuthibitishwa na mkutano mkuu wa chama ngazi ya taifa.

iii) Kanuni zitaonyesha utaratibu wa kuitisha na kuendesha vikao mbalimbali, kuweka akidi na jinsi ya kutunza kumbukumbu za vikao vya chama.

### 29. KUKAIMU UONGOZI

i) Kipindi cha kukaimu uongozi hakitazidi miezi kumi na mbili (12) tangu kukaimiwa kwa nafasi iliyowazi.

ii) Ikiwa nafasi itakuwa wazi kwa kiongozi kuwa masomoni, mgonjwa au kazi nyingine itakayo kubaliwa na chama, nafasi hiyo itakaimiwa hadi hapo atakaporudi.

### 30. KUJAZA NAFASI ZILIZOWAZI KATIKA CHAMA

Utaratibu wa kujaza nafasi zilizo wazi katila chama utafafanuliwa kwenye kanuni za chama.

## 31. KUFUTWA KWA CHAMA

i) Chama hiki kinaweza kufutwa au kufungiwa shughuli zake ikiwa uamuzi huo utakubaliwa na wanachama wote kwa kupiga kura na kukubaliwa na theluthi mbili (2/3) ya wanachama hao.

ii) Baada ya uamuzi wa kufutwa kwa chama, fedha na mali za chama zitagawanywa kwa kuzingatia sheria za nchi au kadri wanachama wenyewe watakavyo ona inafaa.

## 32. MGOMO

Mgomo ni haki ya kila mwanachama katika kushinikiza upatikanaji wa haki, lakini utaitishwa pale tu njia nyingine zote zitakapokuwa zimeshindikana na kabla ya kuitishwa ni lazima utaratibu

uliotajwa na heria uwe umezingatiwa kama itakavyoelekezwa na kanuni za chama.

## KUUNGANA NA KUUNDA SHIRIKISHO

Chama hiki kinaweza kuungana na chama au vyama vingine au kujishirikisha na shirikisho lolote ndani au nje ya nchi ilimradi kama wanachama watakuwa wameridhia.

## SEHEMU YA NANE.

## 33. UFAFANUZI AU FASILI

i) **CHAMA:** Jina la chama hiki litakuwa Chama cha Kulinda na Kutetea Haki za Walimu Tanzania (**CHAKUHAWATA**) kama lilivyo amuliwa na wanachama wenyewe. .

ii) **KATIBA:** Itajulikana kwa jina la **Katiba ya Chama cha Kulinda na Kutetea Haki za Walimu Tanzania (CHAKUHAWATA)** ambayo ndani yake mna kanuni za msingi ambazo zitakiwezesha chama kuendesha shughuli zake.

iii) **KANUNI.** Ni desturi, kawaida au taratibu zilizo za lazima zinazotafsiri katiba hii na kutoa maelekezo ya kutekeleza katiba hii ya chama.

iv) **HAKI.** Ni stahili anayopata mfanyakazi baadaya kutimiza wajibu wake wa kazi.

v) **WAJIBU.** Ni kutenda kazi kwa mujibu wa sheria za kazi bila hiari ili uweze kupata malipo yanayolingana na kazi iliyofanywa.

vi) **TAWI.** Kwa mujibu wa Katiba hii, Tawi ni mahali pa kazi penye wanachama wasiopungua kumi (10) walio katika kata za utawala wa kiserikali.

vii) **KAMATI YA UTENDAJI.** Ni sehemu ya wanachama waliochaguliwa na wanachama wenzao kwa madhumuni ya kusimamia na kuratibu shughuli za chama katika ngazi husika.

viii) **MKUTANO MKUU.** Ni kikao cha juu cha chama chenye kauli na maamuzi ya mwisho katika ngazi husika.

ix) **MWENYEKITI.** Ndiye kiongozi na msemaji mkuu wa chama katika ngazi husika.

x) **KATIBU.** Ni mtendaji mkuu wa shughuli za chama katika ngazi husika.

xi) **MWEKA HAZINA.** Ndye mtunza fedha za chama katika ngazi husika.

xii) **ADA.** Ni malipo yanayotolewa kila mwezi na mwanachama kwa ajili ya uhai na ustawi wa chama.

xiii) **WADHAMINI.** Ni miongoni mwa wanachama waadilifu waliochaguliwa na mkutano mkuu wa taifa na kupewa mamlaka ya kusimamia mali na fedha kwa niaba ya wanachama wote.

xiv) **TAASISI.** Ni mahali pa kazi panaposhughulikia utoaji wa elimu.

xv) **WILAYA.** Ni eneo la kiutendaji la chama kama itakavyo katika maeneo ya kiutawala ya wilaya za kiserikali.

xvi) **MGOGORO**. Ni hali ya kutoafikiana kati ya mwajiri na mwajiriwa, au mwajiriwa na mwajiriwa mwenzake, au chama cha wafanyakazi na mwajiri, au mwanachama na mwana chama.

xvii) **MGOMO**. Ni hali ya wafanyakazi wa mahali fulani kukataa kufanya kazi mpaka masharti fulani yatimizwe kwa kufuata sheria za kazi.

xviii) **MWALIMU**. Ni mfanyakazi yeyote mwenye taaluma ya ualimu na mafunzo ya ualimu au leseni ya kufundishia.

xix) **MFANYAKAZI**. Ni mtu kuwa katika hali ya makubaliano au mkataba wa maandishi na mwajiri kwa kutenda kazi yenye malipo au fidia, ujira au mshahara kwa juma, majuma au mwezi.

xx) **MWANACHAMA**. Ni mfanyakazi aliyejiunga na chama cha wafanyakazi kwa kulipa ada ya kila mwezi au mwalimu mstaafu.

xxi) **SERA**. Ni dira inayotoa mwelekeo na mwongozo wa shughuli zote za chama.

xxii) **UELEDI**. Ni hali ya kuelewa na kufahamu kitu.

xxiii) **KATIBA YA NCHI.** Ni katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.